**Jina……………………………………………………………Nambari yako……………./………**

**Shule…………………………………………………………...Sahihi yako…….…………………....**

**Tarehe ………………………….…...**

**102/2**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 2**

**(LUGHA)**

**MACHI 2013**

**MUDA: SAA 2 ½**

# CROSS COUNTRY JOINT REGISRATION EXAM – 2013

***Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)***

**MAAGIZO**

1. Karatasi hii ina maswali **manne**. (Ufahamu, ufupisho, lugha na Isimu Jamii)

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | | |

***Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa***

***Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.***

**UFAHAMU (Alama 15)**

***Soma kifungu kisha ujibu maswali.***

Vijana ni tegemeo kubwa kwa kila taifa na bila shaka wao ni viongozi wa kesho kama ilivyo msemo wa kawaida.

Isitoshe, takwimu za idadi ya watu hapa nchini Kenya zinoanyesha kuwa idadi ya vijana inachukua asilimia sitini hivi, hii ikiwa ni sehemu kubwa ya wapiga kura ambao uamuzi wao hutupa viongozi, wanasiasa wema na wabaya.

Ndiposa kila taifa lenye maono ya kuwa na maendeleo, lazima liweze kutambua umuhimu wa vijana ambao ni asasi muhimu ya maisha na uongozi wa kesho.

Serikali imejaribu kuanzisha miradi mbalimbali humu chini kwa minajiri ya kuwainua vijana.

Tumeona kazi kwa vijana na kulifurahia wazo nzuri la serikali kuona kwamba vijana wanapata kazi na pato japo kidogo. Lakini mbona ufisadi na ufujaji wa pesa kama hizi umekuwa kama sumu ya kuharibu kilicho kizuri? Tungependa kuona vijana wakishirikishwa katika utenda kazi badala ya kukaa vivi hivi mitaani pasi na kufanya lolote, si mapenzi ya wakenya kuwaona vijana wakiogelea kwenye dimbwi la vileo na madawa ya kulevya.

Taifa letu linawahitaji vijana, siyo tu kwa kutumiwa kuwapigia debe vigogo wa kisiasa lakini tunawahitaji kama mihimili muhimu ya uongozi wa kesho.

Simba akikosa nyama, tumesikia kuwa yeye hula nyasi na mtoto akikosa la mama hata la mbwa huamwa.

Ukosefu wa kazi na hasa kwa vijana limekuwa kama limbukizi la makaa kwenye tanuri ya matatizo kwa vijana na kwa kukosa matumaini, wengi wa vijana wamejitosa kwenye ulevi wa kila aina ya vileo bora tu mtu ajihisi kuwa yupo mbingu ya tatu kama si ya nne.

Hali ya maisha ya vijana imekuwa si hali tena na hasa vijana wanaume. Kwa wale waliooa wamebaki tu kuwa picha kwenye ndoa zao, ulevi umetamalaki maisha yao hivi kwamba hata kupata watoto ni kama tu kuupanda mchongoma.

Kaunti mbalimbali za Kenya zinalia, mabibi wakiwalilia waume wao.

Kila siku imekuwa ni siku ya maandamano, wakiandamana kwa sababu ya pombe haramu ambazo zimewaoa waume zao na kuwafanya watumwa na si watumiwa tu lakini watumwa hanithi ambao hawawezi kupata watoto katika hali zao.

Inafedhehesha kuona hata nyumba nyingi zinaongozwa na kutunzwa na mabibi.

Hivyo basi, kilichobaki ni wakenya wote kwa jumla kuiendeleza na kuiunga mkono sheria ya Mututho, ili tuwaokoe viongozi wa kesho. Asiye sika la mkuu mwishowe…

<u>Maswali</u>

(a) Eleza matatizo yanayokumba juhudi za kuwainua vijana. (al 3)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(b) Kulingana na mwandishi, kwa nini ni muhimu kuwashughulikia vijana? (al 2)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) Mwandishi anamaanisha nini kwa kusema, "imbikizi la makaa kwenye tanuri ya matatizo…?" (al 2)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(d) Kwa vijana ambao ni waraibu wa ulevi, "Kupata watoto ni kama tu kuupanda mchongoma". Eleza. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(e) Pendekeza njia za kusuluhisha tatizo la ulevi kwa vijana. (al 3)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(f) Eleza maana ya msamiati ufutao kama ulivyotumiwa kifunguni: (al 3)

(i) Mihimili ………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………

(ii) Asasi ………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iii)Pigia debe…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

2. **MUHTASARI**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Wasiokuwa na aibu wana mji wao, nani aliwadanganya walimu, wazazi na wanafunzi wa shule zilizohusika na visa vya udanganganyifu kuwa njia bora ya kunadhifisha jina lao ni kushiriki maandamano? Ala! Hata shule ambapo walimu walifumaniwa wakisaidia wanafunzi kudanganya katika mitihani pia zinashiriki maandamano? Kwa maoni yangu haya ni matumizi mabaya ya uhuru wa kushiriki maandamano kwa imani ambayo katiba imewapatia wakenya.

Ilikuwa aibu kubwa kuwaona walimu wakuu waheshimiwa kwenye runinga wakiongoza wazazi na wanafunzi kulikashifu baraza la KNEC. Kwa kuwaadhibu ilhali wao wenyewe wanajua mambo yalivyoenda. Ikiwa uliiba mtihani na hilo lingegunduliwa na kuthibitishwa na KNEC. Suluhu si kuwachosha wazazi na wanafunzi kukimbia na kuimba "haki yetu". Hiyo siyo haki yenu, ni "wizi wenu" na mnapaswa kujifunza kutokana na makosa. Hayo ndio madhara ya kuzoea vya kunyonga badala ya kuchanikia vya kuchinja.

Nani husema kuwa alisema kuwa wakina Omera hawajui Kiswahili? Nani alisema Kiswahili ambayo ni lugha ya kibantu hakiwezi kueleweka na jamii zisizo za kibantu?

Bila shaka shule ya wavulana ya Maranda na ya wasichana ya Kisumu Mkoani Nyanza zimewaonyesha wazi kuwaa si lazima uishi pwani ya Kenya ndipo ujue Kiswhaili sanifu.

Kujua lugha yoyote ile kunahitaji nia, bidii na kujitolea kujifunza sheria na misamiati. Shule za upili za Maranda na ya wasichana ya Kisumu zimeondoa fikira potovu kuwa watu kutoka Nyanza wana Kiswahili kibovu. Matokeo hayo pia yameondoa fikira kuwa Kiswahili ni cha shule za Pwani. Bora uwe na ari na bidii, hakuna kisichowezekana. Haikosi kuwa walimu pia waliweka mipango maalumu kuimarisha matokeo mazuri ya Kiswahili. Kuna haja ya umoja na ushirikiano kati ya walimu na wanafunzi mpaka wakati wafanyapo mtihani. Kukamilisha silabasi mapema, kwa wakati unaofaa, jitihada na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi. Vilevile wanafunzi waunde makundi ya kusoma na kujitolea kujifunza sheria za lugha na misamiati.

***Maswali***

(a) Fupisha aya **nne** za kwanza (maneno 55-60) (al. 8)

**Maandalizi**

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

**Jibu**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

(b) Eleza jinsi matokeo mema katika Kiswahili yalivyopatikana (maneno 40) (al. 7)

***Maandlizi***

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

***Jibu***

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a). i) Taja irabu mbili za mbele (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

ii) Andika mifano miwili ya nusu – irabu. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(b) Tofautisha maana:

i) ba’rabara……………………………………………………………………………

ii) bara’bara…………………………………………………………………………………

(c) Tambua yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi ifuatayo:

Baba aliandikiwa barua na motto wake. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Changanua sentensi ifuatatyo kwa njia ya visanduku

Mwalimu alipomwona jana alimkabidhi zawadi (alama 4

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e) Bainisha matumizi ya ‘ni’ katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mama alituamuru, “Tokeni hapa! Nyini ni wezi.”

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(f) Tunga sensensi mbili kudhihirisha maana tofauti za neon lifuatalo: (alama 2)

Mwiko

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(g) Onysha matumizi mawili ya kibainishi.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(h) Andika kwa msemo wa taarifa.

Mama alimuuliza bintiye, “ Utaenda sokoni kesho?” (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(i) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya kutendama

Maziwa yamenganda (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(j) (i) Unda kivumishi kutokana na kitenzi kifuatacho:

Safisha (ala ma 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Unda nomino kutokana na kitanzi Safiri (alama 1 )

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(k) Eleza matumizi mawili ya – ngali (ala ma 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(I) Bainisha maana mbili za sentensi ifuatayo:

Watu wa Kajiado wamwogopa samba kuliko watu wa Nairobi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(m) Andika Kwa wingi:

Waya umekatika. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(n) Andika kwa wingi:

Sahani yangu ili nunuliwa mjini. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(o) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo:

Watu hao walimba zizuri sana. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(p) (i) Nini maana ya mofimu tegemezi. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Toa mfano wa mofimu tegemezi? (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(q) Andika kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari. (alama 2)

<u>Mwalimu</u> alisoma kwa <u>makini</u>

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(r) Yakinisha sentensi ifuatayo:

Chakula hakipikiki vizuri. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(s) Ainisha nomino katika sentensi ifuatayo:

Urembo wake unatokana na matumizi ya manukato. (ala ma 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII (Alama 10)**

*Soma mazungumzo haya kisha ujibu maswali.*

Kamau: Karibu kastoma.

Chebet: (Akisogea karibu) Asante.

Kamau: Hii ni mia tano, mia tatu nah ii mia.

Chebet: Kwani hakuna ys shilingi kumi?

Kamau: Hei! Wewe huoni dollar imepanda na pia petrol imepanda.

(1) Tambua sajili hii na utoe idhibati. (alama 2)

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

(2) Taja na kueleza sifa nne za mazungumzo haya. (alama 8)

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................